# SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA VIONGOZI WA KITAIFA NAMBA 10 YA 2002 NA KUTUNGA SHERIA INAYOWEKA UTARATIBU WA KUWAENZI VIONGOZI WA KITAIFA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU

**VIFUNGU** **MAELEZO**


**SEHEMU YA KWANZA**
**MASHARTI YA AWALI**

1. Jina fupi na kuanza kutumika.
2. Ufafanuzi.

**SEHEMU YA PILI**
**UHIFADHI WA KUMBUKUMBU NA MAMBO MENGINE**

3. Uanzishwaji wa Makumbusho Maalum.
4. Uhifadhi wa kumbukumbu na mambo mengine.
5. Eneo, Tukio, Taasisi na sehemu ya kutolea huduma kupewa jina la Kiongozi wa Kitaifa.
6. Uwekaji wa kumbukumbu na mambo mengine katika Makumbusho Maalum.
7. Taratibu za kuhifadhi au kuteketeza kumbukumbu na mambo mengine.
8. Wiki ya Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa.

**SEHEMU YA TATU**
**TARATIBU ZA MAZIKO YA KIONGOZI WA KITAIFA, WA JUU NA SERIKALI**

9. Aina za Maziko.
10. Kiongozi anayepaswa kufanyiwa maziko.
11. Uwezo wa Rais.
12. Utaratibu wa maziko.
13. Utaratibu wa Maziko ya Mke au Mume wa Kiongozi Mkuu wa Kitaifa.

14. Taarifa ya Kifo.

15. Maziko na sababu ya kifo.

16. Taarifa ya Mkurugenzi Mkuu.

17. Kipindi cha maombolezi.

18. Kamati ya Maziko ya Kitaifa.

19. Kazi za Kamati ya Maziko ya Kitaifa.

20. Kamati Tendaji ya Maziko.

21. Kazi za Kamati Tendaji ya Maziko.

22. Kamati Nyengine.

23. Eneo, aina ya maziko na Wasia.

24. Utaratibu wa utoaji wa heshima ya mwisho.

**SEHEMU YA NNE**
**MAHITAJI YA FEDHA KWA AJILI YA MAZIKO YA KIONGOZI WA KITAIFA, WA JUU AU KISERIKALI**

25. Fedha kwa ajili ya Maziko ya Kiongozi wa Kitaifa, Kiongozi wa juu au Kiongozi wa Kiserikali.

26. Matumizi ya Fedha.

**SEHEMU YA TANO**
**MASHARTI MENGINEYO**

27. Mwaliko.

28. Makosa yatokanayo na matumizi ya jina, picha, sanamu au taswira ya Kiongozi wa Kitaifa.

29. Taarifa za upotoshaji.

30. Makosa yatokanayo na kuhamisha, kuharibu, kuondosha au kubadili umbo la waraka, kifaa au kitu.

31. Adhabu ya Jumla

32. Kanuni

33. Kufuta na Kubakiza.

**SHERIA NAMBA 5 YA 2019**

**NIMESAINI**

**{DKT. ALI MOHAMED SHEIN}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

21 Oktoba, **2019**

# SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA VIONGOZI WA KITAIFA NAMBA 10 YA 2002 NA KUTUNGA SHERIA INAYOWEKA UTARATIBU WA KUWAENZI VIONGOZI WA KITAIFA NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa, 2019 na itaanza kutumika mara tu itakaposainiwa na Rais.

Ufafanuzi.

**2.** Katika Sheria hii, isipokuwa kama maelezo yatahitaji vyenginevyo:

"Jaji Mkuu" maana yake ni Jaji Mkuu wa Zanzibar;

"Kaburi" maana yake ni sehemu ya ardhi ambayo mwili wa marehemu unazikwa;

"Kamati" maana yake ni Kamati ya Maziko ya Kitaifa, Kamati Tendaji ya Maziko na Kamati nyengine yoyote itakayoanzishwa chini ya Sheria hii;

"Kiongozi wa Kitaifa" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Makamu wa Rais wa Zanzibar ambaye yupo madarakani au amestaafu;

"Kiongozi wa Juu" maana yake ni Jaji Mkuu na Spika wa Baraza la Wawakilishi ambaye yupo madarakani au amestaafu;

"Kiongozi wa Serikali" maana yake ni Waziri, Mwanasheria Mkuu, Naibu Waziri, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Jaji wa Mahakama Kuu, Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Mufti, Kadhi Mkuu na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aliyefariki akiwa madarakani na kwa maana hii inajumuisha mke au mume wa Kiongozi wa Kitaifa ambaye yupo madarakani au amestaafu;

"Kuenzi" maana yake ni kuhifadhi kumbukumbu za kazi za Kiongozi wa Kitaifa na shughuli alizozifanya wakati wa uhai wake pamoja na kumuandalia taratibu rasmi za maziko;

"Makamu wa Rais" maana yake ni Makamu wa Kwanza wa Rais na Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar walioteuliwa kwa mujibu wa kifungu cha 39 (2) cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, na kwa maana hii inajumuisha Waziri Kiongozi Mstaafu;

"Makumbusho Maalum" maana yake ni makumbusho yaliyoanzishwa chini ya kifungu cha 3 cha Sheria hii;

"Mkurugenzi Mkuu" maana yake ni Mkurugenzi Mkuu wa Wizara ya Afya;

"Rais" maana yake ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

"Sehemu ya Ibada" maana yake ni msikiti au kanisa au inajumuisha sehemu nyengine yoyote inayotumika kwa ajili ya ibada;

"Serikali " maana yake ni Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

"Siku ya Karume " maana yake ni siku ya tarehe 7 Aprili ya kila mwaka;

"Spika" maana yake ni Spika wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar;

"Waraka wa Serikali" maana yake ni Waraka wowote uliotajwa chini ya kifungu cha 4(2) (a) cha Sheria hii;

"Wasia" maana yake ni maelezo ya maandishi au matamshi ambayo marehemu ameacha kwamba angependelea au asingependelea vifanyike katika kuenziwa kwake;

"Waziri" maana yake ni Waziri anayehusika na usimamizi wa Sheria hii; na

"Wiki ya Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa" maana yake ni wiki inayoanzia tarehe 1 hadi 6 Aprili ya kila mwaka.

## SEHEMU YA PILI
## UHIFADHI WA KUMBUKUMBU NA MAMBO MENGINE

Uanzishwaji wa Makumbusho Maalum.

**3.** Kunaanzishwa Makumbusho Maalum ya kuhifadhi kumbukumbu na vitu vyengine vya Kiongozi wa Kitaifa ambaye aliwahi kushika wadhifa wa Urais.

Uhifadhi wa kumbukumbu na mambo mengine.

**4.**-(1) Itakuwa ni jukumu na wajibu wa Waziri kusimamia na kudhibiti ukusanyaji, uhifadhi, uondoshaji na kuenzi kumbukumbu, sanamu na vitu vyengine vya Kiongozi wa Kitaifa ambaye amewahi kushika nafasi ya Urais.

(2) Utaratibu wa utunzaji wa kumbukumbu, sanamu na vitu vyengine vya Kiongozi wa Kitaifa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, itajumuisha mambo yafuatayo:

(a) waraka wa Serikali ambao ulitolewa au kutengenezwa kama vile hotuba, picha, kitabu, kabrasha na sheria ambayo ameisaini;

(b) taarifa yoyote ya Serikali iliyotolewa au kupatikana na kuhifadhiwa katika mkanda, video na vyombo vyengine vya kielektroniki;

(c) vitu vya kumbukumbu na mambo kama vile zawadi alizopewa, daftari binafsi, kitu cha madini, nguo au chombo, kitu binafsi, na sanamu kitahifadhiwa kwa kupata ridhaa yake au ridhaa ya familia yake;

(d) maelezo ya kumbukumbu na taarifa zinazohusiana ya kiongozi huyo yatakayotolewa na mtu anayemfahamu;

(e) mali inayohamishika au isiyohamishika inayohusiana na historia ya maisha yake itahifadhiwa kwa ridhaa yake au ridhaa ya familia yake; na

(f) sanamu itakayoonesha sehemu ya juu ya mwili wa Marehemu Sheikh Abeid Amani Karume na maelezo mafupi yanayoelezea kipindi chake cha urais.

(3) Kumbukumbu na mambo mengine yatasimamiwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii na sheria nyengine yoyote inayohusiana na usimamizi wa nyaraka.

(4) Maamuzi yanayohusiana na mgawanyo wa aina za kumbukumbu na mambo mengine au vitu vinavyotaka kuhifadhiwa yatafanywa baada ya kushauriana na kupata ridhaa ya mwakilishi wa familia ya marehemu.

(5) Mtu yeyote ambaye ana vifaa vya kumbukumbu za Kiongozi wa Kitaifa anaweza, kwa ridhaa yake, kuvipeleka vifaa hivyo kwenye Makumbusho Maalum.

Eneo, Tukio, Taasisi na sehemu ya kutolea huduma kupewa jina la Kiongozi wa Kitaifa.

**5.**-(1) Waziri, kwa ridhaa ya Baraza la Mapinduzi, ataita jina la eneo au taasisi kama vile kiwanja cha ndege, kiwanja cha michezo, mtaa, skuli, chuo kikuu, klabu ya michezo, barabara kuu, jengo au tukio kuwa la Kiongozi wa Kitaifa ikiwa ni sehemu mojawapo ya kumuenzi.

(2) Mtu yeyote atakayetaka kulitumia jina la Kiongozi wa Kitaifa kama ilivyoainishwa chini kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, ataomba ridhaa kwa Waziri.

(3) Waziri, baada ya kupokea maombi ya kutumia Jina la Kiongozi wa Kitaifa, atawasilisha maombi hayo Baraza la Mapinduzi kwa ajili ya kuidhinishwa.

Uwekaji wa kumbukumbu na mambo mengine katika Makumbusho Maalum.

**6.**-(1) Kumbukumbu yoyote na mambo mengine ambayo wakati wa kuanza kutumika kwa Sheria hii, alipewa, ilitolewa, au kukabidhiwa Kiongozi wa Kitaifa kwa niaba ya Serikali au Serikali ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania au sehemu nyengine yoyote nje ya Zanzibar, pale itakapohitajika yatahifadhiwa katika Makumbusho Maalum.

(2) Mtu mwengine yeyote anayemiliki kumbukumbu hiyo au kitu chengine kwa ajili ya matumizi ya umma au binafsi kitabakia katika miliki yake hadi wakati ambao mtu huyo ataamua kutoa, kukabidhi au kuiuzia Serikali ambapo baadae kitahifadhiwa katika Makumbusho Maalum.

Taratibu za kuhifadhi au kuteketeza kumbukumbu na mambo mengine.

**7.**-(1) Waziri, baada ya kushauriana na waziri anayehusika na usimamizi wa kumbukumbu za umma na nyaraka, atashauri kuhusu taratibu maalum za kuhifadhi au kuteketeza kumbukumbu na mambo mengine au kitu ambapo:

(a) ushauri wa ziada uliopatikana kutoka kwa mwakilishi wa familia ya Kiongozi wa Kitaifa, na ikaonekana kwamba kumbukumbu au kitu hicho kina maslahi maalum kwa nchi na kwamba kuhifadhiwa kwake ni lazima katika Makumbusho Maalum; au

(b) mashauriano na mwakilishi wa familia ya Kiongozi wa Kitaifa yamefanyika, na ikaonekana kwamba kumbukumbu au kitu hicho hakina maslahi maalum kwa nchi na kwamba uteketezaji wake ni wa lazima.

(2) Uhifadhi na uteketezaji wa kumbukumbu, waraka, kifaa au kitu chengine utakuwa kwa mujibu wa Kanuni zitakazotungwa chini ya Sheria hii.

Wiki ya Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa.

**8.**-(1) Kutakuwa na Wiki ya Kuwaenzi Viongozi wa Kitaifa kuanzia tarehe 1 hadi 6 Aprili ya kila mwaka.

(2) Siku ya tarehe 7 Aprili ya kila mwaka itakuwa ni siku ya Karume ambayo itakuwa ni siku ya mapumziko na Waziri kwa kushauriana na Baraza la Mapinduzi ataainisha pahala patakapofanyika shughuli za kumbukumbu za siku hiyo.

(3) Siku ya Karume itakuwa ni siku ya kumbukumbu ya marehemu Sheikh Abeid Amani Karume ambapo kutafanyika shughuli mbalimbali za kuashiria kukumbukwa mafanikio mazuri ya utendaji wake.

## SEHEMU YA TATU
## TARATIBU ZA MAZIKO YA KIONGOZI WA KITAIFA, WA JUU NA SERIKALI

Aina za Maziko.

**9.** Kutakuwa na aina mbili za maziko, maziko ya kitaifa na maziko ya kiserikali kwa mujibu wa hadhi ya kiongozi kama ifuatavyo:

(a) Maziko ya kitaifa yatafanywa kwa taratibu zilizoelezwa chini ya kifungu cha 12 (1), (2), (3), (4), (5), (7) na (8) cha Sheria hii kwa heshima ya Kiongozi wa Kitaifa au Kiongozi wa Juu ambaye wakati wa kifo chake alikuwa madarakani au amestaafu; na

(b) Maziko ya Kiserikali yatapangwa kulingana na Kiongozi wa Serikali ambaye wakati wa kifo chake alikuwa madarakani.

Kiongozi anayepaswa kufanyiwa maziko.

**10.**-(1) Kiongozi anayestahiki katika mpango wa maziko uliotajwa chini ya Sheria hii atakuwa Kiongozi wa Kitaifa, Kiongozi wa Juu au Kiongozi wa Serikali na taratibu za maziko zitafanywa kuendana na hadhi ya kiongozi kama ifuatavyo:

(a) Rais ambaye amefariki akiwa madarakani au ambaye amestaafu atafanyiwa maziko ya kitaifa kama ilivyoelezwa katika kifungu 12 (1), (2) na (3) cha Sheria hii;

(b) Makamu wa Rais ambaye amefariki akiwa madarakani au ambaye amestaafu atafanyiwa maziko ya kitaifa kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 12 (4) cha Sheria hii;

(c) Kiongozi wa juu atafanyiwa maziko ya kitaifa kama ilivyolezwa katika kifungu cha 12(5) cha Sheria hii;

(d) Kiongozi wa Serikali ambaye amefariki akiwa madarakani atafanyiwa maziko ya Kiserikali kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 12(6), (7) na (8) cha Sheria hii;

(e) Rais aliyeondoshwa kwa azimio la kumuondoa Rais madarakani lililopitishwa na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hatoingia katika utaratibu wa maziko kwa mujibu wa Sheria hii;

(f) Rais ambaye amejiuzulu na hakukaa katika nafasi hiyo kwa kipindi cha miaka mitano lakini ametumikia kwa kipindi cha miaka mitatu au zaidi taratibu za maziko yake yatakuwa sawa na Makamu wa Rais kama ilivyoelezwa chini ya kifungu cha 12(4) cha Sheria hii;

(g) Makamu wa Rais ambaye uteuzi wake umefutwa na Rais au amejiuzulu kabla ya kumaliza miaka mitano lakini katumikia zaidi ya miaka mitatu taratibu za maziko yake zitakuwa sawa na Waziri kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 12(6) cha Sheria hii.

(h) Kiongozi wa Juu ambaye amejiuzulu kabla ya kutimia miaka mitano lakini ametumikia zaidi ya miaka mitatu, maziko yake yatakuwa sawa na Waziri kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 12(6) cha Sheria hii.

(2) Mpango wa maziko kwa Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi au Jaji wa Mahakama Kuu utafanywa na Ofisi ya Spika au Jaji Mkuu kwa mpangilio kama itakavyoonekana inafaa.

Uwezo wa Rais.

**11.** Bila ya kuathiri masharti ya kifungu cha 9 cha Sheria hii, mtu yeyote ambaye hakustahiki katika utaratibu wa maziko kama ilivyoelezwa chini ya Sheria hii, Rais anaweza kuagiza marehemu azikwe kiserikali.

Utaratibu wa maziko.

**12.** -(1) Kutakuwa na gwaride maalum la Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania siku ya kuzikwa kwa Rais aliyefariki akiwa madarakani au Rais aliyestaafu, gwaride hilo litakuwa lenye gadi moja ambalo litafanywa karibu na eneo la kuzikia.

(2) Gwaride hilo litaandaliwa na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania.

(3) Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania litapiga mizinga ishirini na moja hewani karibu na eneo la kuzikia wakati wa maziko.

(4) Makamu wa Rais ambaye amefariki akiwa madarakani au aliyestaafu, ataandaliwa gwaride la Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania lenye gadi moja na kupigiwa mizinga kumi na tisa hewani karibu na eneo la kuzikia wakati wa maziko.

(5) Endapo Kiongozi wa Juu amefariki, atastahiki gwaride la Jeshi la Polisi la Tanzania lenye gadi moja na kupigiwa risasi baridi kumi na saba hewani karibu na eneo la kuzikia wakati wa maziko.

(6) Hakutokuwa na Gwaride wala kupiga risasi baridi hewani kwa maziko ya Kiongozi wa Serikali atakayefariki akiwa madarakani.

(7) Wasifu wa marehemu utasomwa katika eneo la kuzikia.

(8) Dua ya kumuombea marehemu itasomwa kwa mujibu wa dini au itikadi yake.

(9) Jeneza la marehemu litafunikwa Bendera ya Zanzibar kwa mujibu wa hadhi ya Kiongozi aliyetajwa katika kifungu cha 9 (a) na (b) cha Sheria hii, isipokuwa kwa jeneza la Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi ambalo litafunikwa bendera ya Baraza hilo.

(10) Bila ya kuathiri masharti ya kifungu hiki, iwapo kiongozi aliyefariki alitumikia Serikali na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, taratibu za Maziko na ufunikwaji wa Bendera katika Jeneza la marehemu itafanyika baada ya Mashauriano Baina ya Kamati ya Maziko ya Kitaifa ya Serikali na Kamati ya Maziko ya Kitaifa ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

(11) Bendera iliyotumika kufunika jeneza la Rais aliyefariki akiwa madarakani au aliyestaafu, itakabidhiwa kwa Mkurugenzi mwenye dhamana ya Mambo ya Nje aliyepo Zanzibar na baadae kuhifadhiwa katika Makumbusho Maalum, na kwa Kiongozi mwengine wa kitaifa bendera ya Zanzibar itakabidhiwa kwa familia ya marehemu.

Utaratibu wa Maziko ya Mke au Mume wa Kiongozi wa Kitaifa.

**13.** Mke au Mume wa Kiongozi Mkuu wa Kitaifa aliyefariki maziko yake yatakuwa sawa na maziko ya Kiongozi wa Serikali aliyefariki akiwa madarakani.

Taarifa ya Kifo.

**14.**-(1) Mara tu baada ya Rais kupokea taarifa ya kifo cha Kiongozi wa Kitaifa, ataitisha kikao cha Baraza la Mapinduzi na kuwaalika Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania waliopo Zanzibar na Wakuu wa Idara Maalum za Serikali na kufanya yafuatayo:

(a) kuwasilisha taarifa maalum ya kifo cha marehemu inayoelezea muda na sababu ya kifo;

(b) kutangaza kipindi cha maombolezi na kupeperusha bendera nusu mlingoti; na

(c) kutangaza kifo hicho katika vyombo vya habari.

(2) Pale ambapo Kiongozi wa Kitaifa amefariki ndani ya nchi, Waziri husika katika ofisi ambayo marehemu alifanyia kazi atawajibika kutoa taarifa rasmi kwa Rais au mtu anayeshika dhamana za Rais kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya 1984 na pale ambapo Kiongozi wa Kitaifa atafariki akiwa nje ya nchi, Ubalozi wa Tanzania wa nchi aliyofariki Kiongozi huyo utawajibika kutoa taarifa hiyo kwa Rais.

(3) Pale ambapo Rais amefariki, siku ya maziko yake itakuwa ni siku ya mapumziko kwa ajili ya maombolezo.

(4) Pale ambapo kitatokea kifo cha Kiongozi wa Kitaifa, Rais akiwa hayupo ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au hayupo katika majukumu ya kazi kwa sababu yoyote, mtu anayeshika dhamana za Rais atatoa taarifa za kifo.

(5) Pale ambapo Rais aliyepo madarakani amefariki, Makamu wa Pili wa Rais ataitisha kikao cha Baraza la Mapinduzi na kuwaalika Wakuu wa Jeshi la Ulinzi na Usalama wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania waliopo Zanzibar na Idara Maalum za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na kutoa taarifa kama inavyojieleza katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki.

(6) Pale ambapo Kiongozi wa Serikali amefariki, Makamu wa Pili wa Rais atamjuulisha Rais na atatoa tangazo la kifo katika vyombo vya habari vya umma baada ya kupokea taarifa ya kifo kutoka kwa familia ya marehemu.

Maziko na sababu ya kifo.

**15.**-(1) Maziko ya Kiongozi anayehusika kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii, yatafanywa kulingana na dini, madhehebu, mila, desturi, itikadi na wasia wa marehemu kwa kuzingatia sababu na mazingira ya kifo chake.

(2) Pale ambapo mwili wa marehemu haukupatikana kutokana na kifo cha ajali ya ndege, kifo cha majini au sababu nyengine yoyote, shughuli za maziko zitakazofanyika ni maombolezo na matendo ya kidini yatakayofuatiwa na dua kulingana na dini ya marehemu kama itakavyoamuliwa na Kamati ya Maziko ya Kitaifa.

Taarifa ya Mkurugenzi Mkuu.

**16.** Atakapofariki Kiongozi wa Kitaifa kutokana na ugonjwa wowote ambao maziko yake yatahitaji ushauri wa Mkurugenzi Mkuu, ushauri wake utazingatiwa chini ya Sheria hii.

Kipindi cha maombolezo.

**17.** Kipindi cha maombolezo kitategemea na wadhifa wa Kiongozi aliyefariki na kitakuwa kama ifuatavyo:

(a) kwa Rais aliyepo madarakani, kipindi cha maombolezo kitakuwa kwa muda wa siku kumi na nne na bendera itapepea nusu mlingoti;

(b) kwa Rais aliyestaafu, kipindi cha maombolezo kitakuwa kwa muda wa siku saba na bendera itapepea nusu mlingoti;

(c) kwa Makamu wa Rais ambaye yupo madarakani, kipindi cha maombolezo kitakuwa kwa muda wa siku saba na bendera itapepea nusu mlingoti;

(d) kwa Makamu wa Rais aliyestaafu, kipindi cha maombolezo kitakuwa kwa muda wa siku tatu na bendera itapepea nusu mlingoti;

(e) kwa Kiongozi wa Juu ambaye yupo madarakani, kipindi cha maombolezo kitakuwa kwa muda wa siku tatu na bendera itapepea nusu mlingoti; na

(f) kwa Kiongozi wa Serikali aliyetajwa katika Sheria hii, kipindi cha maombolezo kitakuwa ni siku ya maziko na bendera haitapepea nusu mlingoti.

Kamati ya Maziko ya Kitaifa.

**18.** -(1) Kunaanzishwa Kamati ya Maziko ya Kitaifa ambayo Mwenyekiti wake atakuwa Makamu wa Pili wa Rais.

(2) Wajumbe wa Kamati ya Maziko ya Kitaifa ni wafuatao:

(a) Waziri anayehusika na maziko ya Kiongozi wa Kitaifa ambaye atakuwa Makamu Mwenyekiti;

(b) Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;

(c) Waziri mwenye dhamana ya Tawala za Mikoa na Idara Maalum za Serikali;

(d) Mkurugenzi mwenye dhamana ya Mambo ya Nje Zanzibar;

(e) Wakuu wa Vikosi vya Ulinzi na Usalama wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania waliopo Zanzibar;

(f) Wakuu wa Idara Maalum za Serikali;

(g) Waziri mwenye dhamana ya fedha;

(h) Waziri mwenye dhamana ya habari; na

(i) Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi.

(3) Katibu Mkuu anayehusika na Wizara inayosimamia shughuli za maziko ya Kiongozi wa Kitaifa, atakuwa ni Katibu wa Kamati ya Maziko ya Kitaifa.

(4) Bila kuathiri kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki kutakuwa na Sekretarieti ya Kamati ya Maziko ya Kitaifa itakayoongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara inayoshughulikia maziko ya Viongozi wa Kitaifa au Kiongozi wa Kiserikali na Mkurugenzi wa Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa ambaye atakuwa Katibu.

(5) Isipokuwa kwamba, iwapo Makamu wa Pili wa Rais anashikilia Madaraka ya Rais, Waziri anayehusika na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais atakuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kitaifa ya Maziko.

Kazi za Kamati ya maziko ya Kitaifa.

**19.** Kamati ya Maziko ya Kitaifa itakuwa na kazi zifuatazo:

(a) kusimamia taratibu zote za maziko ya Viongozi wa Kitaifa, Viongozi wa Juu na Vongozi wa Serikali;

(b) kutoa taarifa kwa Rais kila baada ya muda kutegemea na matukio tofauti yanayohusu maziko;

(c) kuthibitisha gharama za maziko;

(d) kupokea muongozo kutoka kwa Rais na kuziwasilisha katika Kamati Tendaji ya Maziko;

(e) kuielekeza Kamati Tendaji ya Maziko kwa ajili ya kuratibu shughuli za maziko;

(f) kupokea na kujadili taarifa na mapendekezo kutoka katika Kamati Tendaji ya Maziko;

(g) kuwasiliana na familia ya merehemu kuhusu taratibu za maziko; na

(h) kupokea ripoti ya Maziko na kuiwasilisha Serikalini.

Kamati Tendaji ya Maziko.

**20.** -(1) Kunaanzishwa Kamati Tendaji ya Maziko itakayoongozwa na Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi.

(2) Wajumbe wa Kamati Tendaji ya Maziko watakuwa:

(a) Katibu Mkuu wa Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ambaye atakuwa Makamu Mwenyekiti;

(b) Wakuu wa Vikosi vya Ulinzi na Usalama wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania waliopo Zanzibar;

(c) Wakuu wa Idara Maalum za Serikali;

(d) Mkurugenzi wa Mambo ya Nje aliyepo Zanzibar;

(e) Katibu Mkuu anayehusika na masuala ya fedha;

(f) Katibu Mkuu wa Wizara inayohusika na mawasiliano na usafirishaji;

(g) Katibu Mkuu wa Wizara inayohusika na Tawala za Mikoa na Idara Maalum za Serikali;

(h) Katibu wa Baraza la Wawakilishi;

(i) Katibu Mkuu wa Wizara inayohusika na Habari;

(j) Mtendaji Mkuu wa Mahakama; na

(k) Kiongozi wa dini ya marehemu ndani ya Zanzibar.

(3) Katibu Mkuu anayehusika na Wizara inayoshughulikia maziko ya Kiongozi wa Kitaifa, atakuwa ni Katibu wa Kamati Tendaji ya Maziko.

Kazi za Kamati Tendaji ya Maziko.

**21.** Kamati Tendaji ya Maziko itakuwa na kazi zifuatazo:

(a) kutayarisha na kuwasilisha makadirio ya matumizi ya maziko husika katika Kamati ya Maziko ya Kitaifa;

(b) kufanya mipango ya maziko na kuongoza shughuli za maziko;

(c) kutoa mwongozo kwa kamati nyengine au kamati zitakazoanzishwa na Waziri kuhusiana na maziko;

(d) kuandaa ratiba ya shughuli za maziko;

(e) kuwasilisha taarifa za shughuli za maziko kwa Kamati ya Maziko ya Kitaifa; na

(f) kuandaa taarifa ya maziko.

Kamati Nyengine.

**22.** Kamati Tendaji ya Maziko inaweza kuanzisha kamati nyengine itakapoona kuna ulazima wa kufanya hivyo.

Eneo, aina ya maziko na Wasia.

**23.**-(1) Familia ya marehemu itaamua kuhusu eneo la kuzikia na ikiwa marehemu ameacha wasia kuhusu eneo au namna anavyotaka kuzikwa.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, Kamati ya Mazishi ya Kitaifa itapanga pahala na taratibu za mazishi kwa Kiongozi wa Kitaifa ambapo baadhi ya shughuli za Serikali kuhusu mazishi hayo zitafanyika.

(3) Kiongozi wa Kitaifa anaweza, akiona inafaa, kuandika wasia kuhusu mazishi yake na kuwasilisha nakala katika Ofisi ya Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi.

(4) Wasia ulioachwa na marehemu utaandikwa na yeye mwenyewe wakati akiwa hai nakala hiyo inatakiwa iwasilishwe Ofisi ya Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi.

Utaratibu wa utoaji wa heshima ya mwisho.

**24.**-(1) Jeneza la mwili wa Kiongozi wa Kitaifa aliyefariki akiwa madarakani au amestaafu, Kiongozi wa Juu au Kiongozi wa Serikali aliyefariki akiwa madarakani litawekwa sehemu itakayoamuliwa na Kamati ya Maziko ya Kitaifa kwa ajili ya jamii kuweza kutoa heshima ya mwisho wakiongozwa na viongozi wa dini kuu zilizopo Zanzibar.

(2) Kipindi cha kutoa heshima ya mwisho kitategemea dini, wasia wa marehemu na maamuzi ya Kamati ya Maziko ya Kitaifa lakini hakitazidi siku tatu.

(3) Jeneza la mwili wa marehemu litachukuliwa kutoka eneo alilopatiwa heshima ya mwisho kuelekea sehemu ya ibada na baadae litachukuliwa kuelekea eneo la maziko.

## SEHEMU YA NNE
## MAHITAJI YA FEDHA KWA AJILI YA MAZIKO YA KIONGOZI WA KITAIFA, WA JUU AU KISERIKALI

Fedha kwa ajili ya Maziko ya Kiongozi wa Kitaifa, Kiongozi wa Juu au kiserikali.

**25.** Fedha kwa ajili ya shughuli za maziko ya Kiongozi wa Kitaifa, Kiongozi wa Juu au Kiongozi wa Serikali, ambao wametajwa katika Sheria hii, zitatoka katika Mfuko Mkuu wa Serikali kwa mpangilio ufuatao:

(a) Katibu wa Kamati ya Maziko ya Kitaifa atawasilisha maombi ya fedha kwa Katibu Mkuu wa Wizara inayosimamia masuala ya fedha kwa kuzingatia shughuli zitakazofanyika; na

(b) Katibu Mkuu wa Wizara inayosimamia masuala ya fedha atalazimika kutoa fedha na zitatumika kwa njia ya masurufu.

Matumizi ya Fedha.

**26.** -(1) Fedha zilizoombwa kutoka Mfuko Mkuu wa Serikali zitatumika kwa ajili ya:

(a) kusafirisha mwili wa marehemu na vitu vitakavyohitajika kwa ajili ya maziko; na

(b) matumizi ya mahitaji yote kwa ajili ya kufanikisha maziko ya Kiongozi wa Kitaifa, Kiongozi wa Juu au Kiongozi wa Serikali.

(2) Matumizi yote yatafanyika kwa mujibu wa masharti yaliowekwa na Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma na Sheria ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma au sheria nyengine yoyote.

## SEHEMU YA TANO
## MASHARTI MENGINEYO

Mwaliko.

**27.** Mwenyekiti wa Kamati ya Maziko ya Kitaifa au Mwenyekiti wa Kamati Tendaji ya Maziko anaweza kumualika mtu yeyote kushiriki katika Kamati anayoiongoza akiona kuna ulazima wa kufanya hivyo.

Makosa yatokanayo na matumizi ya jina, picha, sanamu au taswira ya Kiongozi wa Kitaifa.

**28.** Mtu atakayetumia jina, picha, sanamu au taswira ya Kiongozi wa Kitaifa kwa shughuli yoyote bila ya ruhusa ya Waziri atakuwa ametenda kosa na atakapopatikana na hatia, atalazimika kulipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Mbili za Kitanzania au kifungo cha miezi sita au atatumikia adhabu zote mbili kwa pamoja faini na kifungo.

Taarifa za upotoshaji.

**29.** Mtu yeyote atakayetoa taarifa za uongo kuhusiana na kifo cha Kiongozi wa Kitaifa, atakuwa ametenda kosa na iwapo atatiwa hatiani atalazimika kulipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Mbili za Kitanzania au kifungo cha muda usiopungua miezi kumi na mbili au atatumikia adhabu zote mbili kwa pamoja faini na kifungo.

Makosa yatokanayo na kuhamisha, kuharibu, kuondosha au kubadili umbo la waraka, kifaa au kitu.

**30.** Mtu yeyote ambaye, bila ya ridhaa au ruhusa ya jamaa wa marehemu:

(a) ataondoa waraka, kifaa au kitu;

(b) atahamisha au kusafirisha waraka, kifaa au kitu;

(c) ataiba waraka, kifaa au kitu;

(d) atabadilisha umbile au kuharibu waraka au sanamu, taswira, kifaa au kitu;

(e) atauza waraka au kifaa au kitu; au

(f) atanakili waraka, kifaa au kitu;

kuhusiana na Kiongozi wa Kitaifa, Kiongozi wa Juu au Kiongozi wa Serikali atakuwa ametenda kosa na atakapopatikana na hatia, atalazimika kulipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Mbili za Kitanzania au kifungo cha miezi sita au atatumikia adhabu zote mbili kwa pamoja faini na kifungo.

Adhabu ya Jumla.

**31.** Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria hii, kwa adhabu ambazo hazijaainishwa, atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atatozwa faini isiyopungua Shilingi Milioni Tatu za Kitanzania au kifungo kisichopungua mwaka mmoja au atatumikia adhabu zote mbili faini na kifungo.

Kanuni.

**32.**-(1) Waziri anaweza kutunga Kanuni kwa madhumuni ya utekelezaji mzuri wa Sheria hii.

(2) Bila ya kuathiri masharti ya jumla ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki,Waziri anaweza kutunga kanuni:

(a) zinazoelezea utaratibu wa kuzipatia jina la Kiongozi wa Kitaifa, taasisi za ndani na nje kwa mujibu wa kifungu cha 5 cha Sheria hii;

(b) zinazoelezea utaratibu wa uanzishaji na usimamizi wa Makumbusho Maalum iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 3 cha Sheria hii; na

(c) zinazoelezea utaratibu wa ukusanyaji, uhifadhi au uteketezaji wa kumbukumbu na vitu vyengine kama inavyoelezwa chini ya kifungu cha 6 na 7 cha Sheria hii.

Kufuta na Kubakiza.

**33.**-(1) Sheria ya Kuwaenzi Viongozi namba 10 ya 2002 inafutwa.

(2) Bila ya kujali kufutwa kwa Sheria chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kitu chochote kilichofanywa au hatua iliyochukuliwa chini ya masharti ya Sheria iliyofutwa itachukuliwa kuwa imefanywa chini ya masharti ya Sheria hii.

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 18 Septemba, 2019.

..................................................
(RAYA ISSA MSELLEM)
***Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.***